Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Falsafa ya Jazanda ya Uongozi na Mauko katika Methali za Jamii ya Wanyore: Mtazamo wa Kisemantiki

**Henry F. Andele[1]; Susan C. Choge[2]; Fred S. Wanjala[3]**
**[1,2] Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya**
**[3]Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya**
**Main author email: andelehenry@yahoo.com**

## IKISIRI

Makala hii inatokana na utafiti ambao uliazimia kutathmini falsafa ya jazanda katika methali za Wanyore kwa mtazamo wa kisemantiki. Madhumuni ya makala yenyewe yanahusu falsafa ya uongozi na mauko katika methali za Wanyore. Nadharia ya Uhusiano ya Sperber na Wilson (1986) na iliyoendelezwa nao (2004) ndiyo iliyoongoza makala hii. Nadharia hii ilitumiwa kufafanulia maana za methali katika jamii ya Wanyore. Data ilikusanywa kutoka kwa Wanyore wanaoishi katika kaunti ndogo ya Emuhaya na Luanda katika kaunti ya Vihiga. Makala haya yalitumia njia za uchanganuzi matini na mahojiano kukusanya data. Vifaa vilivyotumiwa vilikuwa ratiba ya usaili na tepurekoda. Data ilichanganuliwa kimaelezo kwa kunukuu methali za Kinyore, kisha zikatafsiriwa na kufasiriwa katika Kiswahili hatimaye falsafa ya jazanda ya uongozi na mauko ikaainishwa na kuelezwa. Matokeo ya kazi hii yatachangia kueleweka kwa falsafa ya jazanda ya uongozi na mauko miongoni mwa wanajamii. Pia, yatakuwa nyongeza ya marejeleo kwa watafiti katika uwanja wa methali.

**Maneno muhimu:** falsafa, jazanda, mauko, kisemantiki

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Andele, H.F., Choge, S.C. & Wanjala, F. S. (2020). Falsafa ya Jazanda ya Uongozi na Mauko katika Methali za Jamii ya Wanyore: Mtazamo wa Kisemantiki. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 163-172

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Fasihi simulizi hubuniwa na kuhifadhiwa akilini mwa wanajamii walizozibuni. Aina hii ya fasihi iliwasilishwa na kusambazwa kwa njia ya mazungumzo ya kisanaa, kughani, kuigiza, kuimba hata kwa ulumbi au kuikariri katika hadhira hai katika miktadha mbalimbali. Mabadiliko katika fasihi simulizi na hasa kipera cha methali ndicho kinachosababisha hitaji la kukusanya na kujadili falsafa ya jazanda ya uongozi na mauko katika methali za Wanyore. Maitaria (2019) anafafanua methali kuwa semi teule zinazotumiwa na watu katika uwasilishaji, ubainishaji na uelekezaji wa masuala muhimu ya jamii. Methali huibua masuala muhimu katika jamii kupitia falsafa ambazo zimekitwa ndani yake.

Dai kuu la makala haya ni kwamba methali za Wanyore zimesheheni falsafa ya uongozi na mauko ambazo zinaweza kutazamwa kwa mtazamo wa kisemantiki katika miktadha ya jamii hii. Pamoja na kujadili falsafa hizi, mstakabali wa methali katika jamii umejadiliwa. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ukifuatiwa na njia za ukusanyaji data, nadharia ya utafiti na hatimaye ufafanuzi wa dhana 'falsafa' na 'falsafa katika methali za Wanyore'. Sehemu ya sita inajadili uchanganuzi na matokeo ya utafiti. Hatimaye, tunahitimisha kwa kuangazia mustakabali wa methali katika jamii ya Wanyore. Pamoja na kujadili falsafa hizi, mustakabali wa methali katika jamii umejadiliwa. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ukifuatiwa na njia za ukusanyaji data, nadharia na hatimaye ufafanuzi wa dhana 'falsafa' na 'falsafa katika methali za Wanyore'. sehemu ya sita inajadili uchanganuzi na matokeo ya utafiti. Hatimaye, tunahitimisha kwa kuangazia mustakabali wa methali katika jamii ya Wanyore.

**Njia za Ukusanyaji Data**

Utafiti ulishirikisha Wanyore ambao ni wazawa na wazungumzaji wa lugha ya Kinyore wanaopatikana katika kaunti ndogo za Emuhaya na Luanda ambao waliteuliwa kimaksudi. Uteuzi wa kiupokezano ulitumiwa kuwafikia watu walio na umilisi mkuu katika methali za Kinyore na falsafa yake ambao ni nadra kupatikana. Kwa njia hii, Mmilisi wa kwanza kufikiwa aliombwa kuelekeza mtafiti kwenye wale wengine kama wao hadi wakafikia 17. Uteuzi faafu ulitumiwa kuteua na kushirikisha washiriki wote waliopatikana katika shughuli halisi za kiutendaji katika jamii kama vile: mabaraza ya machifu na manaibu wao, harusi na matanga.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Nadharia ya Uhusiano**

Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986) na wakaiendeleza (2004) ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Nadharia hii ilitumiwa kufafanulia maana za methali katika jamii ya Wanyore. Kadhalika, ilitumiwa kueleza na kufasili hali za kimawasiliano katika methali za Wanyore.

**Dhana ya Falsafa na Falsafa katika Methali**

Falsafa ni mtazamo wa maisha unaohusisha tabia inayohitajiwa katika maisha ya wanajamii husika. Falsafa ni mwongozo wa hekima na busara ambao hutumiwa na wanajamii katika miktadha mbalimbali ya maisha yao. Ni kutokana na hali hii ndipo utafiti huu ukaangazia falsafa ya uongozi na mauko katika jamii ya Wanyore.

Methali ni semi au kauli teule zinazotumiwa na watu katika uelekezaji, ubainishaji na uwasilishaji wa masuala muhimu ya jamii. Katika mapokeo ya jamii methali zimetumiwa kama vielelezo vya hisia, itikadi, maono na pia katika ubainishaji kwa utaratibu kuhusu maisha ya watu (Masolo, 1994). Hivyo basi, methali ni zao halisi la jamii na kanzi mojawapo katika uhifadhi na uwasilishaji wa tamaduni za jamii. Kila jamii ina methali zake ambazo huwa nembo ya kutambulisha kikundi cha watu. Ujumbe katika methali huweza kufasiriwa kwa njia ya moja kwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

moja au kupitia kwa mafumbo, kutokana na ruwaza ya tamathali za semi zinazotokana na mazingira ya jamii husika (Maitaria, & Momanyi, 2016). Katika mawasiliano ya jamii, methali husaidia kubainisha fikra za watu kuhusu mafikira ya kiulimwengu kwa njia ambayo inaafiki malengo, matakwa na matarajio yao katika jamii. Kwa hivyo, methali katika jamii ya Wanyore ni kielelezo na vipumuzi vya utamaduni wa watu. Licha ya kutilia pondo mazungumzo, methali za Wanyore ni chombo cha kubainishia falsafa ya Wanyore kwa kuzingatia tajiriba na uhalisia wa maisha ya watu katika miktadha ya kihistoria ya jamii. Hivyo basi methali zinapotumiwa kubainika katika muktadha ambamo zimetumika, huibua na huielekeza mijadala ambayo ina azma ya kufikia maamuzi fulani kuhusu masuala yanayowahusu watu katika jamii hiyo.

Wamitila (2008) anafafanua methali kuwa semi zinazopokezanwa, zinazofahamika na zinazoelezea ukweli ambao huwa unakubalika na jamii inayohusika. Methali katika jamii hujikita katika utamaduni, mila na mielekeo ya jamii inayohusika kwa kushugulikia masuala mbalimbali.

Vilevile methali inaweza kufafanuliwa kama msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu au uzito, wenye muundo au sifa za kishairi, unaokusudiwa kuadhibu au kuelekeza na kushauri (Wamitila, 2001). Maitaria (2019) anatambua kwamba wenyeji wa bara la Afrika wana mwono mmoja wa falsafa unaofasiriwa kwa kuzingatia utamaduni wanaouenzi. Jamii ya Wanyore ikiwa mojawapo ya jamii za Kiafrika, ingali na matumizi ya methali na zingali zina nafasi na jukumu katika kufanikisha falsafa ya jamii hii. Ni katika falsafa hizi ambamo mila na utamaduni wa jamii ya Wanyore umekitwa. Falsafa hizi zinasheheni mielekeo, mitazamo, maono, mila na utamaduni wa jamii ya wanyore na kupitia kwazo, Wanyore ni mwonoulimwengu kwao. Yaani jamii hii ya Wanyore inatumia methali kama njia mojawapo ya kuutazama au kuelezea ulimwengu ama mazingira wanamoishi.

Ili kuelewa falsafa katika jamiii ya Wanyoore kupitia methali, methali hizi zinahitajika kufafanuliwa na kuelezwa kwa wanajamii. Kwa hivyo, ni muhimu kutaja hapa kuwa methali hutolewa kama kauli ambazo zinarejelea hali fulani ya maisha katika jamii ya Wanyore. Methali hizi zinaashiria mtazamo wa jamii kuhusu mazingira wanamoishi kwani huchota picha zake katika mazingira ya kimaumbile, vitu na fikra zinazozunguka jamii, utamaduni na maisha ya watu katika jamii.

Imedhihirika kwamba methali si maneno matupu hata ingawa methali yaweza kuwa imeundwa kwa maneno ya kawaida na lugha nyepesi. Jambo muhimu linalofaa pia tuzingatie ni kwamba methali ni sanaa ya maneno inayosanifu amali za jamii inayohusika kama zifanyavyo tanzu zingine za fasihi. Sanaa iliyomo katika methali hufundika busara au hekima yenye mafunzo muhimu katika uhalisi kwa maisha ya watu (Mulokozi & Kitogo, 2007). Kwa hali hii, kila uwanja wa maisha ni kisima cha kuundia methali.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Falsafa ya Uongozi na Mauko katika Methali za Wanyore

#### Uongozi

Uongozi ni dhana au taaluma inayompa mhusika madaraka na uwezo wa kuwawezesha wale wanaoongozwa naye kuunganisha nguvu, stadi na vipaji vyao na kuvitumia ili kufikia malengo yao (Wikipedia 2020). Jamii ya Wanyore ilisheheneza falsafa ya uongozi wa kifamilia na wa kijamii katika methali mbalimbali kama vile:

(i) Uongozi wa Kifamilia

Dhana ya uongozi wowote ule hustahili kuanzia nyumbani. Katika jamii ya Wanyore, kiongozi bora



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ni yule ambaye ana uwezo wa kuongoza familia kwa mujibu wa kaida, mila na desturi za jamii hiyo. Hii ndiyo ngazi ya kwanza ambapo kiongozi anatathminiwa iwapo anaweza kupewa nafasi ya kuongoza jamii. Uongozi wa familia unajitokeza katika methali mbili zifuatazo:

1. ***Oburele bwaula so*** (Tafsiri: Utelezi ulimubwaga babako)

Jazanda ipo katika neno "oburele" katika Kiswahili ni utelezi ni hali tete isiyotabirika."So" ni baba yaani kiongozi wa familia. Maana yake ni kuwa, kwa kawaida kiongozi wa familia hutegemewa kama nguzo na hatarajiwi kushindwa katika majukumu yake. Hata hivyo, wakati mwingine kiongozi anayetegemewa na watu wengine katika majukumu yake yote, hufika wakati ambapo inabidi naye atafute ushauri kutoka kwa wengine kwani hakuna anayejua kila kitu. Hali hiyo ndiyo inayoweza kumfanya kujirekebisha na kusonga mbele katika utekelezaji wa majukumu yake ya uongozi. Aghalabu, hali unayodharau ndiyo inayoonyesha udhaifu wako.

Wanaoongozwa wasishangae endapo mtu anayewaongoza atateleza au atakosea katika utenda kazi wake au katika jukumu lake. Heshima au mtazamo wa watu kuhusu kiongozi usibadilike kutokana na udhaifu unaotokea mara moja au mara chache. Hii inatokana na hali kwamba, kila binadamu ana udhaifu wake. Muktadha ni wa uongozi. Matumizi ni kuwa endapo kiongozi katika familia hususan baba hatatekeleza majukumu yake ipasavyo asilaumiwe kwa sababu ni mwanadamu kama wengine. Kwa wale wanaoongozwa, wasiwadharau viongozi wao kutokana na kasoro ndogo ndogo kwa mfano, kushindwa katika jambo ni kawaida, watu hujifunza kutokana na makosa mathalan, baba anapaswa kuheshimiwa na mkewe na watoto wake kwani kifamilia ndiye kiongozi akisaidiwa na mkewe. Endapo atakosea, ashauriwe wala si kwa kukejeliwa kwani akidharauliwa, atakosa kujiamini na atapoteza ukakamavu wake kutekeleza majukumu yake. Basi, katika matumizi ya methali hii inasisitizwa kuwa wanaoongozwa wawe tayari kumtetea kiongozi wao kwa vyovyote vile mbele ya watu licha ya kuwa ameteleza na ametenda visivyo.

2. O***mwana wa mbeli ne eshiekhoyelo*** (*Tafsiri: Mwana wa kwanza au kifungua mimba ni wa kujivunia)*

Jazanda **hapa ni ipo katika neno "omwana" kwa kurejelea kifungua mimba maana inajikita hapa ni kitu au mradi wa kwanza au maendeleo au ufanisi wa kwanza**

Maana ni kuwa mtoto wa kwanza ni kichocheo cha furaha katika familia na hupewa malezi ya kutosha. Katika utamaduni wa Wanyore, ndoa isiyo na mtoto haikukamilika. Mtoto ni kiungo muhimu katika familia hususan wa kwanza. Muktadha ni wa ufanisi wa kwanza au uzazi wa kwanza au mke au mume wa kwanza au mradi wa kwanza.

Matumizi ni mwana wa kwanza huthaminiwa sana na hushughulikiwa kikamilifu maana yake wazazi wao huwa bado vijana au huwa na hamu ya kuanzisha familia na mara nyingi huwa na muda na rasilmali za kumlea. Mtoto wa kwanza ni kama kioo kwa watoto wengine watakaozaliwa, hivyo kila juhudi hufanywa ili asipotoke kimadili. Inaaminika kuwa akiwa mwadilifu, wengine pia watafuata mkondo uo huo. Yaani wataweza kuleleka vizuri wakiiga mfano wa yule wa kwanza. Mtoto wa kwanza ndiye aliyekuwa kama kielelezo na mfano wa kuigwa katika familia. Aidha, akipotoka wale wengine pia nao watakosa mwelekeo na familia pia inaweza kusambaratika kwa sababu wadogo wake hawatakuwa na mfano mwema wa kuiga.

Pamoja na fahari, cheo, mamlaka yanayotokana na uongozi, kuna changamoto kadhaa. Watu wanaoongozwa hutarajia mengi kutoka kwa viongozi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wao ilhali mengine huwa ni vigumu kuyatekeleza. Kiongozi hususan wa kitamaduni alihitaji kuwa na sifa teule ili kumudu hali za waliokuwa chini yake. Sifa kama ukarimu, upole, ukakamavu na kutolipiza kisasi zilikuwa muhimu. Kiongozi alifaa kuwa mtu wa kusamehe bila masharti. Jamii haikosi watu waliopotoka kimaadili, kiongozi bora alihitajika kuwa na hekima ya kuweza kutatua masuala mbali mbali katika jamii. Isitoshe, kiongozi alihitajika kukabiliana na hali zote katika jamii ziwe mbaya au zenye changamoto. Jamii iliundwa na familia mashinani, madhali familia ndio kiungo muhimu katika jamii. Katika familia baba ndiye kiongozi na anategemewa kwa kutoa mwelekeo, ushauri na ufadhili.

Mtazamo wa jamii kuhusu utawala na uongozi ni mambo yaliyoenda au yaliyofanywa sambamba kwa kuwa yana uhusiano wa karibu sana japo utawala una dhana ya kulazimisha. Katika tamaduni za Wanyore mume katika familia alikuwa na usemi wa mwisho na neno lake lilikuwa kama sheria. Ni muhimu kutaja hapa kuwa katika ulezi baba ambaye ni mzazi wa kiume alishirikiana na mama (mzazi wa kike) katika kuwalea watoto wao, bila ushirikiano watoto walikuwa na tabia isiyolingana na matarajio ya jamii. Hata hivyo, si ajabu wakati mwingine alilemewa katika uongozi wake wa kifamilia. Iwapo ingetokea hivyo mkewe aliwaendea mashemeji zake hususan wakubwa wa mumewe kiumri ili waweze kutoa mwelekeo kwa familia yake. Hao walikuwa jukumu la kuelekeza familia na kuhakikisha kwamba uelekezi ufao unatekelezwa ili familia ya ndungu yake ipate msingi imara.

Katika familia zote mwana wa kwanza alichukuliwa kama mzazi na wadogo wake. Alikuwa kiongozi kwa wale wadogo na aliheshimiwa sana. Alihitajika kuwa kielezo kwao na hata angewaadhibu ilipohitajika. Endapo baba mzazi angefariki, alijukumika kusimamia familia iliyowachwa na baba. Wakati wa kugawa shamba, mwana wa kwanza wa kiume alipata mgao mkubwa kuliko wengine wote, vivyo hivyo hali ilikuwa hivyo katika ugavi wa mali nyinginezo zote. Vile vile mke au mume kwanza alithaminiwa sana katika jamii. Kutokana na hali hii hata mume akioa mke mwingine na kwa bahati mbaya aage atazikwa kwa mke wa kwanza. Kisa na maana ni yule wa kwanza ndiye baado anatambuliwa kama mke wake. Vivyo hivyo, hata mke akimtaliki mume wake kwanza na iwe haikufanywa kirasmi na apoteze maisha yake atazikwa kwa mume wake wa kwanza. Kwa jumla jamii ilithamini na kuienzi kitu chochote cha kwanza. Inadhihirika katika falsafa hii kuwa kiongozi yeyote alitarajiwa kuwa mvumilivu na kuwaelewa waliokuwa chini yake. Hakutarajiwa kuwa na pupa katika kuwashughulikia watu au familia yake. Familia ilichukuliwa kuwa kiungo cha kimsingi sana ambapo uongozi unaanzia. Kutokana na hali uongozi ulisisitizwa kuanzia katika familia. Iliaminika kwamba mtu akilelewa vyema, ataweza kuajibikia familia nzima.

(ii) Uongozi wa Kijamii

Falsafa ya uongozi imeweza kudhihirika katika methali zifuatazo;

3. ***Emichela chibukananga munyaanza, nebutswa siichulanga tawe*** (Tafsiri: Mito hutiririsha maji baharini, lakini bahari haijai wala kuvunja kingo zake.)

Jazanda hapa ipo katika neno "emichela" kwa Kiswahili ni mito na maana inayojitokeza hapa ni watu wanaoongozwa au wananchi wa kawaida. "Chibukananga"ni kukutana hata hivyo jazanda iliyoko hapa ni ya maji kwa kuashiria Changamoto , matatizo au matukio mbali mbali. "Munyanza"kwa bahari maana ya ndani ni kiongozi au wakuu au watu wenye mamlaka fulani katika jamii. "Siichulanga" ni kujaa dhana ambayo imejificha hapa ni kwamba mambo kuharibika, kuchoka au kulemewa. Maana ya bahari haijai hata inapopokea maji kutoka kwa mito na endapo itajaa ni kwa muda mfupi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

sana, hatimaye hurejelea hali ya kawaida. Kama vingozi watu wengine wote huelekeza matatizo yao kwao,hawafai kulalamika au kuchoka, ndio hali ya maisha na ndio uongozi. Kuna baadhi ya mambo ambayo licha ya kuwa ni mema au yana umuhimu si lazima tujishughulishe nayo au wakati mwingine viongozi kuwalazimishia watawaliwa vitu ambavyo si muhimu kwao. Muktadha ni kuwa uongozi au utawala. Matumizi ni kwamba utawala na uongozi katika jamii. Uongozi huhitaji uvumilivu na kutenda haki kwa wote. Viongozi kuanzia kwa baba na mama kwa boma lazima wawe na hekima na wawe tayari kushughulikia maslahi ya walio chini yao pasi na minong'ono.

4. ***Eiana eyanilanga tsiosi*** (Tafsiri: Anapolia hulilia wote)
**Jazanda hapa inadhihirika katika neno *Eiana* ambalo moja kwa moja linaashiria ng'ombe maana ya ndani ni mtu mmoja katika kundi ambaye huwakilisha wengine wote wakati anapowasilisha hoja fulani katika jamii. *Eyanilanga ni kulia kwa ng'ombe wakati wa hitaji fulani lakini maana iliyoko hapa ni kuwa kuzungumza au kulalamika kwa madhumuni ya kutaka* kushughulikiwa.** Maana ing'ombe maana ya ng'ombe anapotoa ishara ya kutaka kushughulikiwa malishoni, ng'ombe wote watafaidika, si yeye pekee yake. Hivi ni kusema kuwa katika mahali popote pale hususan palipo na mkusanyiko wa watu, kuna yule anayeongea kwa niaba ya wengine ili kushughulikiwa. Muktadha ni wa uongozi au mahitaji au uhitaji. Matumizi ni kuwa iwapo wewe ni mwakilishi wa watu, usiwe na ubinafsi ikiwa ni kushughulikiwa ushughulikie wote bila kubagua. Falsafa hapa ni kuwa katika jamii sharti kuwe na muakilishaji watu. Watu wote hawawezi kuzungumza kwa wakati mmoja. Ni wajibu wa kiongozi kuongozwa na haki na ukweli ili watu wote waweze kunufaika katika jamii. Hali hii basi inahitaji uajibikaji wa hali juu kwa kiongozi ili asiwe anajishulikia kwa maisha yake ya kibinafsi. Kupitia methali hii falsafa ya jamii ni kwamba sharti kuwe na kiongozi ambaye anategemewa na kuajibikia wengine katika jamii. Kiongozi huyu ndiye hutoa ulekezi na ushauri kwa niaba ya jamii nzima.

5. ***Linani liabolela olwanda mbu kata noholela oulie!*** (Tasfiri: Jitu liliambia jabali hata kama limenyamaza limesikia!)

**Jazanda ipo katika "linani"kwa Kiswahili ni jitu ni mshauri au aliye na hekima**. "olwanda" kwa Kiswahili ni **jabali hapa kwa maana ya mtu mwenye mapuuza**. Maana hapa ni kuwa tushauri wote, hata kama wengine watapuuza tujiondoe lawamani. Muktadha ni wa wosia au mawaidha. Matumizi ni kuwa iwapo umejukumiwa kutoa ushauri au mawaidha, fanya hivyo bila kujali anayeyazingatia na asiyeyazingatia. Pia, katika jamii iliaminika kwamba kuna watu ambayo ni watundu, wakaidi, wenye mapuuza na kwa vyovyote vile hawataki kufuata kaida za jamii. Kiongozi wa jamii aliwajibikia wote kwa kuwaelekeza hata wale wasiotaka kufuata na kutii kaida na desturi za jamii. Hali hii ilisisitizwa kwa sababu wasije kupata nafasi ya kumlaumu yeyote katika jamii.

**Mauko**
Mauko yamejitokeza katika methali kama hali ya kukatiza tamaa na vile mauti au kifo kinachompata binadamu moja kwa moja katika jamii kama inavyojitokeza katika methali zifuatazo:
Methali zinazorejelea falsafa ya mauti zimejitokeza katika miktadha tofauti tofauti ambayo ni pamoja na:
**Muktadha wa Ushujaa**

*Amatsi keranga omwelema* (Tafsiri: Maji humuua baharia)

**Jazanda inajitokeza katika neno "omwelema" kwa baharia kwa kumaanisha kwamba ni mweledi wa kufanya jambo au shujaa. "Amatsi"ni maji kurejelea hali au mkutadha unaohitaji watu wataalam au jambo tata. "Keranga" ni kuua kwa ya kushindikana.** Maana hapa ni



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kuwa huwezi kushinda katika hali zote kuna siku utashindwa kutekeleza jambo ambalo kwako ni mazoea kulifanya kwa urahisi. Licha ya uzoefu alionao mtu katika fani fulani huenda akashindwa wakati mmoja. Hakuna ubingwa katika kila jambo. Muktadha ni kuwa jambo ambalo kwako kulifanya ni kwa urahisi na imezoeleka. Matumizi ya methali hii ni kwa mashujaa au weledi wa kutenda jambo si ajabu wasifikirie wamekamilika huenda wakaaibika au wakashindwa kutekeleza wajibu waliouzoea. Mtu anaweza kuwa shujaa au mweledi wa kufanya jambo lakini hali ikawa kinyume wakati mwingine anaweza kushindwa kabisa kulifanya jinsi anavyotarajiwa na wengine. Kwa mfano, shujaa wa uogeleaji anaweza akashindwa hadi akasombwa na maji na hata akafa au dereva aliye na tajriba ya miaka mingi huweza kusababisha ajali mbaya au mpiganaji hodari katika jamii ipo siku anaweza kushindwa katika vita na taji lake kunyakuliwa na mtu mwingine. Timu kubwa katika jamii inayoheshimika na inayowachezaji wazuri inaweza kushindwa na timu ndogo.

**Muktadha wa Tahadhari**

***Omufu yeera omulamu*** (Tafsiri: Mfu alimuua mzima au aliye hai)

**Jazanda inajitokeza katika neno "omufu" maana yake kwa Kiswahili ni mfu ni jambo lisilo na faida. Katika neno "omulamu"ni mzima (mtu) ni kuwa ashughulikiaye jambo lililo na athari hasi. Nalo neno "yeera" ni kuua maana ya kuwa na athari hasi.** Maana yake ni kuwa Iwapo kuna jambo au hali tete, hatupaswi kuendelea kwani katika kufanya hivyo tutajiathiri sisi wenyewe kwa mfano, kuchochea ghasia za kijamii. Katika kumshughulikia mfu au mgonjwa au yeyote anyehitaji msaada ni vyema kuwa na tahadhari,kuepuka kuathirika au athari. Mfu amemaliza yake, au amemaliza kuishi na hana haja ya kuishi tena. Muktadha wake ni kwamba hali hasi inayoweza kurudisha nyuma maendeleo kwa mfano, ufisadi au kushughulikia mradi uliokwama au usioharibika au kushughulikia jambo lililoharibika. Matumizi ni kuwa tujaribu tuwezavyo kupinga vita na maovu kwa sababu tukiendeleza yatatuathiri. Wale ambao ni waokoaji wakati wa hali ya dharura kama vile janga la mafuriko wawe makini kwani wao pia wanaweza kujikuta katika hali kama ya waathiriwa.

Muktadha wa Utafutaji Riziki

***Utaamba olafwa*** (Tafsiri: Taabika, lakini usife)

**Jazanda hapa imejikita katika neno "olafwa" kutokufa dhana ya mtu mtu kufariki au kutofariki haipo hapa ila inamaanisha kwamba mtu anaposhughulika katika katika maisha yake ,kuna hali au mambo mengine yakawa magumu mno lakini binadamu kwa vyovyote vile hafai kukata tamaa.Anapaswa kung'ang'ana, kutia bidii na kujipa ili aweze kufaulu.** Maana hapa ni kuwa kufa ndiko kubaya ingawa ni lazima, si kama kutaabika, taabu zina mwisho, kufa ni mwisho wa maisha. Mtu mzima anaposhughulikia aliyekufa huenda akahasirika ama kudhurika katika shughuli hizo. Muktadha ni wa mahangaiko katika kutafuta riziki. Matumizi ni kuhimiza wanaotaabika wasife moyo, kwani shida zina mwisho. Falsafa ya jamii kuwa kukata tamaa katika maisha ni jambo mbaya. Kila mwanajamii anahitajika kujipa moyo ili aweze kupiga hatua za kimaendeleo katika maisha yake. Ikiwa kila mtu atakuwa subira hata janga linamkumba liwe kubwa kiasi kipi litakuja kwisha wakati fulani. Basi kilicho muhimu katika maisha ya kila mwanajamii ni kutafuta mbinu, mikakati na njia mwafaka ya kubiliana tatizo au hali inayomkumba katika maisha yake.

**Muktadha wa Maafa**

***Amasika sikawestanga tawe*** (Tafsiri: Matanga hayaishi)

**Jazanda hapa ipo katika neno "amasika" ambalo ni matanga yake ni janga au mkosi.** Maana yake ni matanga yana athari mbaya kiasi kwamba kurudia hali ya kawaida kwa waliofiwa ni muhali. Mabadiliko yanayofuata huwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ya kudumu. Muktadha ni wa janga au mkosi au msiba. Matumizi ni kuwa mabadiliko yatokanayo na msiba au janga yeyote hulemaza maisha ya kawaida kwa muda mrefu. Falsafa ya jamii ni kuwa katika maisha kuna maafa ambayo yanawakumba waja. Majanga haya huwa mazito mno na mara nyingi si rahisi kuyastahimili na kuweza kuyapitia au kuyashinda au kuyakubali. Hivi ni huwa ni pigo kubwa zaidi na wakati mwingine maisha huenda yasirejelee jinsi yalivyokuwa hapo awali. Mtu anapokumbana na hali nyingine ngumu,hukumbuka hali nyingine tofauti hasa vile ambavyo maisha yalikuwa mazuri kabla ya pigo au mkasa huo kutokea. Himizo, ushauri na falsafa kwa wanajamii ni kuwa hata ingawa kumbukizi hizi zipo na wakati mwingine ni muhali kusaulika ,muhimu ni kwamba lazima mtu ajikakamue na kuweza kuendelea na maisha.

**Muktadha wa Ujasiri au Kuliwaza**

> ***Kata mumasika, batsekhaanga*** (Tafsiri: Hata matangani, watu hucheka)

**Jazanda hapa inadhihirika katika neno "mumasika" kwa matanga ni janga au tatizo sugu. "batsekhanga"ni kucheka ni kujiliwaza au kujifariji.** Maana ni katika msiba, kuna matukio au mazungumzo yanayosababisha furaha japo kwa muda. Muktadha ni wa huzuni au masikitiko. Matumizi ni katika kushughulikia waliofiwa au waliofikwa na mikasa wowote na heri kuwafariji na kukubali yaliyotokea kwani kikasa huwakumba watu wote. Falsafa ya jamii ni hata jambo liwe ngumu kiasi kipi, mtu anahitaji kujipa ujasiri wa hali juu. Majanga yapo na yatakuwepo katika maisha. Kilichomuhimu zaidi ni kujipa ujasiri wa hali juu. Ndipo wanasema hata katika "matanga watu hucheka" ni kwamba huwezi kamwe kuhuzunika au kusononeka milele, mtu huhitaji kujaribu katika maisha yake kuendelea na kutafuta njia mbadala ya kuendelea kuishi.

**Muktadha wa Janga**

> ***Amasika nobwailo*** (Tafsiri: Matanga ni zamu)

**Jazanda hapa ipo katika neno "amasika" kwa matanga maana ni kuwa tatizo au janga au mkosi. Nalo neno "nobwailo" huweza kuwafika watu kwa zamu; leo kwa mmoja kesho kwa mwingine.** Maana yake ni kwamba matanga huwafika au huwakumba watu wote , kila kiumbe kitakufa na kuondoka duniani. Kifo ni tukio la lazima, tusifanye masihara mtu anapoaga dunia. Kando na mauti au kifo inarejelea changamoto za kimaisha ambazo humpata kila mja katika maisha yake. Hivi kwamba leo la mfika fulani na siku nyigine mwingine. Basi ukawa ni kuwa tusipoteze imani au matumaini katika maisha kila siku tujipe moyo kwa hali zote ambazo zinatuathiri katika maisha yetu. Muktadha ni wa janga linalokumba watu. Matumizi ni kuwa wanajamii wanaonywa dhidi ya kufurahia matatizo yanayoathiri wenzao. Wenzao wanapoathirika ni jukumu la kila mmoja kushirikianna na kumsaidia mwenzke kwa kila hali ili angalau awe na nafuu. Wanajamii wawe na hisia kwa wenzao wanapokumbwa na matatizo.

Falsafa inayojitokeza katika methali hii ya 'Amasika nobwailo' ina dhana kuwa wakati ambapo mtu hufikwa na jambo fulani kwa mfano matanga au mkasa wa aina yoyote ile, wanajamii au mtu hafai kufurahia au kuchukulia kama mzaha au masihara. Huu ndio wakati wa wanajamii kushirikiana ili kumfariji na kulitatua tatizo la mwenzao. Ni tahadhari kubwa kuwa mkasa huu umemfika mwenzako leo nawe kesho huenda ukaathirika. Ikiwa ulimsuta au kufurahia hali mbaya iliyomkumba mwenzako wakati huo huo ungekumbushwa jambo kama hilo ambalo lilimpata mwingine na jinsi ambavyo ulivyo onyesha hali ya kutokuwa na huruma au kufurahia hali hiyo. Basi wanajamii wakawa wanatahadharishwa kwamba kifo au janga ni la kila mmoja katika jamii na wanajamii wawe na hekima kila wanaposhughulikia janga lolote lile ambalo limemfika mwanajamii mwenzao.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Jamii ya Wanyore iliamini kuwa kifo hakikutokea kwa sababu Mungu alipanga hivyo bali kifo au mauko yalisababishwa na nguvu za giza au shetani au Miungu yenye nia mbaya kwa mfano, unapoogelea na kwa bahati mbaya uzame basi miungu ya mauti au shetani wamesababisha kifo chako.Hata kama umekongwa sana, ukongwe hausababishi mauti. Iwapo unamshughulikia marehemu huenda akasababisha mauko yako. Kwa mfano, wachimba kaburi wanaweza kushambuliwa na kuuwa na wanyama mwitu, kwa kuwa katika enzi hizo, kaburi lilichimbwa usiku.

Kwa mantiki hiyo, kilichukuliwa kuwa adui mkubwa na kila juhudi ilifanywa kukiepuka jambo ambalo mpaka sasa haliwezekani. Jamii iliamini na ingali inaamini kuwa kifo kilitokea athari zake haziwezi kuisha na jamaa za mwendazake kila mara huomboleza japo kimya kimya.Si ajabu, wengine huja matanga baada ya hata miaka kadhaa.Utamaduni wa kumpa mtoto mchanga jina la mwendazake ni namna maoja ya kuomboleza. Nyakati hizo, mtu alikuwa hatajwi akiwa hai.

Utamaduni wa kurithi wajane ilikuwa kuhakikisha watoto wa marehemu hawakutaabika kwa kumpoteza baba yao. Hii pia ilikuwa namna ya kumkumbuka na kumheshimu mwendazake, hali ya kuendelea kuomboleza.Ili kupunguza, makali ya msiba halikuwa jambo la ajabu kuwa na sarakasi au mchezo wa kuigiza kumkumbuka marehemu kwa mfano, iwapo mwenda zake alikuwa mwanamiereka hodari, watu waliandaa mchezo huo kabla ya kumzika na iwapo alikuwa mlevi, walevi walitumia hafia hiyo kulewa chakari na hata kumwaga kidogo karibuni mwa marehemu. Falsafa ya jamii ya Wanyore inayojitokeza kuhusiana na mauti au mauko nikwamba ingawa kifo ni tukio la kusikitisha maisha lazima yaendelee. Kwa kufanya kila juhudi kuitunza familia ya marehemu.

**Hitimisho**

Methali za Wanyore zinahifadhi falsafa katika muktadha wa utamaduni wa jamii. Ufafanuzi wa methali umejengeka katika tajriba za wanajamii na shughuli za kila siku za maisha yao kwa hivyo huhusisha masuala ambayo ni mwonoulimwengu wao. Hii inatokana na hali kwamba zimetokana na mazingira halisi na hivyo hutumiwa kuwasilisha masuala muhimu. Kutokana na hali hii inabainika kwamba methali ni fasihi hai inayoendeleza shughuli za maisha ya kila siku ya Wanyore na hivyo basi itaendelea kutekeleza wajibu huo hata siku za baadaye.

**Mapendekezo**

Makala haya yamezingatia falsafa ya jazanda katika methali za Wanyore kwa mtazamo wa kisemantiki, ninapendekeza utafiti zaidi kufanywa kuchunguza maana ya miiko ya Kinyore na semi nyingine ya kitamathali kwa kutumia utambuzi au umaizi kutoka kwa falsafa ya kisasa ya lugha.

**MAREJELEO**

Maitara, J.N. (2019). Methali za Kiswahili kama wenzo wa Kubainishia Falsafa ya Kiafrika Kuhusu Familia. Katika Athumani, S. P. na Zuhura, A. B. (wah.). *Koja la Taaluma za Insia: Kwa Heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla.* Dar-es-salaam. Karljamer Publishers Limited. Kur. 435-458.

Maitaria, J.N. na Momanyi, C. (2016). Visawe katika Methali Tafsiriwa za Kiswahili. Katika Jilala, H. (mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company. Kur. 279-293.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Dec-2020|
Received: 01.12.2020; Accepted 02.12.2020; Published on 15.15.2020 at www.editoncpublishing.org
Andele, H.F., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Masolo, D.A. (1994). *African Philosophy in search of Identity.* Bloomington: Indian University Press.

Mulokozi, M. na Kitogo, S. (2007). *Mithali na Mifano ya Kiswahili – Shaaban Robert.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. na Kitogo, S. (2007). *Mithali na Mifano ya Kiswahili – Shaaban Robert.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Sperber, D. na Wilson, D. (1986). *Relevance: Communication and Cognitive.* Oxford: Blackwell.

Wamitila, K.W. (2001). *Archetypal Criticism of Kiswahili Poetry*. Bayreuth: Bayreuth African Studies Series 57.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~Muwa.

Wikipedia. (2020). Maana ya Uongozi. Retirved from https://sw.m.wikipedia.org/wiki/uongozi#maana_ya_uongozi



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org